# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

NambariyaSimu: 2230814/5
Nambariya Fax: 2233722

OFISI YA RAIS - IKULU
S. L. P 2422
ZANZIBAR - TANZANIA.

**18 Novemba, 2020**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kesho Alkhamis tarehe 19 Novemba 2020 anatarajiwa kutangaza Baraza jipya la Mawaziri la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika hafla maalum itakayofanyika Ikulu mjini Zanzibar saa 4:00 asubuhi.

Matangazo ya Baraza jipya la Mawaziri yatatangazwa moja kwa moja kupitia vyombo mbali mbali vya habari na mitandao ya kijamii ikiwemo ZBC Redio na TV, Channel Ten, Face Book ya Ikulu Habari na Youtube ya Ikulu Zanzibar.

Uteuzi wa Baraza jipya la Mawaziri unafuatia uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi uliopita, ambapo Dk. Hussein Ali Mwinyi kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) alichaguliwa kushika wadhifa huo baada ya kupata asilimia 76.27 ya kura.

Kabla ya uteuzi wa Baraza jipya la Mawaziri, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameshamteua Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dk. Mwinyi Talib Haji. Vile vile ameshamteua Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar Bwana Nahaat Mohammed Mahfoudh na Katibu wa Rais wa Zanzibar Bwana Suleiman Ahmed Saleh.

**Imetolewa na**

...............................

**Hassan K. Hassan**
**Mkurugenzi**
**Idara ya Mawasiliano na Habari – Ikulu**

Scanned by TapScanner